Workers Compensation Fund

FIDIA

eNewsletter

TOLEO LA KWANZA I JANUARI - MACHI 2024

# WAAJIRI WATAKIWA KULINDA HAKI ZA WAFANYAKAZI WAO KWA KUWASAJILI WCF




info@wcf.go.tz




Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano kwa Umma WCF:





**Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)**

Jengo la Kambarage,
Ghorofa ya 3,
S. L. P 329, 41104 Dodoma.



**TIMU YA WAHARIRI**

MWENYEKITI;
**Dkt. John Mduma**

MHARIRI;
**Laura Kunenge**

WACHANGIAJI;
**Mcharo Mrutu**
**Meseka Kadala**
**Sophia Mtakasimba**

# Ujumbe kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu



**Dkt. John Mduma**

*Mkurugenzi Mkuu*

**Mpendwa Msomaji wetu,**

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) ni taasisi ya hifadhi ya jamii iliyoanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi [Sura 263] kwa lengo la kushughulikia masuala ya fidia kwa wafanyakazi waliopo katika sekta ya umma na binafsi Tanzania Bara ambao wataumia, kuugua ama kufariki kutokana na kazi wanazozifanya kwa mujibu wa mikataba ya ajira zao. WCF ilianza rasmi kutekeleza majukumu yake tarehe 1 Julai 2015 kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na.105 la 2011.

Miongoni mwa vipaumbele vya WCF ni kutoa elimu kwa wadau wake kuhusu huduma inazozitoa ikiwa ni pamoja na manufaa anayoweza kupata mfanyakazi ambaye atapata madhila ya kuumia, kuugua ama kufariki kutokana na kazi anazofanya. Manufaa hayo ni pamoja na huduma ya matibabu; fidia ya ulemavu wa muda; fidia ya ulemavu wa kudumu; malipo kwa msaidizi anayemhudumia mgonjwa; huduma za utengemao; msaada (rambirambi) wa mazishi; na malipo kwa wategemezi endapo mfanyakazi atafariki.

Kwa mtazamo huohuo wa kutoa elimu kwa wadau, Mfuko umeamua kuanzisha Jarida la ***"Fidia eNewsletter"*** ambalo litapatikana kwa njia ya mtandao kupitia majukwaa mbalimbali ya mtandaoni. Jarida hili litakuwa likitoka kila robo mwaka.

Na kwa namna ya kipekee napenda kuwakaribisha rasmi kusoma toleo la kwanza la Jarida hili ambalo limeangazia habari na matukio mbalimbali muhimu ambayo Mfuko umeyafanya au kutekeleza katika kipindi cha kati ya mwezi Januari hadi Machi, 2024.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kuendelea kutuunga mkono katika shughuli kutoa huduma bora za fidia kwa wafanyakazi wa sekta ya umma na binafsi nchini.

Tunaazimia kuendeleza mafanikio yetu na kuimarisha zaidi huduma zetu ili kukidhi matarajio ya wadau wengine. Tunajivunia kufanya kazi na kujitolea kwa dhati kwa lengo la kuhakikisha ustawi na haki kwa kila mfanyakazi ambaye atapata changamoto ya ajali, kuugua au kifo wakati wa kutekeleza majukumu ya kikazi. Daima tutaendelea kutekeleza majukumu yetu kwa kuzingatia na kuhakikisha upatikanaji wa "Fidia stahiki na kwa wakati" kwa walengwa wa huduma zetu.

Pamoja na Jarida hili, tunawaalika pia kutembelea tovuti yetu www.wcf.go.tz, kurasa zetu za mitandao ya kijamii ya Facebook na Instagram kwa anuani ya Wcf_tz kwa ajili ya kupata Habari mbalimbali kuhusiana na kazi mbalimbali tunazozifanya. Tunapokea pia ushauri na maoni mbalimbali kuhusiana na maudhui ya jarida letu hili kupitia njia za mawasiliano zitakazooneshwa kwenye jarida hili.

**Karibuni.**

> "FIDIA STAHIKI KWA WAKATI"

# Waajiri watakiwa kulinda haki za wafanyakazi wao kwa kuwasajili WCF




Jaji Kiongozi Mhe. Mustapher Siyani, akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo au kikaokazi hicho

Na **Mwandishi wetu.**

Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mhe. Mustapher Siyani amewahimiza waajiri nchini kujisajili na kutoa taarifa za ajira za wafanyakazi wao kwenye Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) ili kulinda haki za wafanyakazi hao pindi wanapopatwa na majanga wakiwa kazini.

Mhe. Jaji Siyani ameyasema hayo mjini Songea, Februari 9, 2024, wakati akifungua kikao kazi cha mafunzo kuhusu sheria ya fidia kwa wafanyakazi kwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Divisheni ya Kazi kutoka Kanda ya Kusini, watendaji wa mahakama na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) kilichoandaliwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

"Pamoja na uwepo wa sheria inayowabana waajiri wanaoshindwa kuwasajili wafanyakazi wao WCF lakini bado kuna waajiri ambao hawatoi taarifa za ajira za wafanyakazi wao na hivyo kuuweka Mfuko katika nafasi ngumu ya kutekeleza majukumu yake," alifafanua Jaji Siyani.

Jaji Siyani alitoa mfano wa kisa cha mfanyakazi mmoja aliyekuwa akifanya kazi kwenye kampuni moja ya ujenzi mkoani Lindi ambaye aliumia akiwa kazini na kupelekea kupoteza baadhi ya viungo vyake na hivyo kumsababishia ulemavu wa kudumu kwa zaidi ya asilimia 75 lakini alikosa vigezo vya kupata fidia kutoka WCF kwa kuwa mwajiri wake hakuwa amejisajili na kuwasilisha michango kwa mujibu wa sheria.

"Licha ya kijana huyo kufanya kazi kwa zaidi ya miaka miwili lakini taarifa zake hazikuwepo WCF na hivyo kukosa haki ya kupata fidia yoyote," alieleza Jaji Siyani na kuongeza kuwa iwapo zingekuwepo taarifa za mfanyakazi huyo, bila shaka angepata fidia bora zaidi ya ile iliyotokana na majadiliano na maridhiano na mwajiri wake.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, alisema Mahakama ya Tanzania ni wadau muhimu wa Mfuko huo katika utekelezaji wa majukumu yake kwa kuwa Mfuko unategemea maamuzi mbalimbali ya mahakama katika utekelezaji wake wa majukumu ikiwemo maamuzi ya kesi za mirathi.

Dkt. Mduma alisema mafunzo hayo ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya Serikali yanayozitaka taasisi zake kuhakikisha zinashirikiana kwa karibu kwa dhumuni la kuongeza tija na huduma bora kwa wananchi.

Pia, aliongeza kuwa mafunzo hayo yanatoa fursa ya kubadilishana uzoefu baina ya wataalam wa Mahakama na WCF kupitia mada mbalimbali zinazowasilishwa ambapo washiriki wanaweza kuja na mapendekezo yatakayoboresha utendaji kazi wa Mfuko huo.

"Ni matarajio yangu kuwa mafunzo haya yataleta manufaa makubwa kwa pande zote mbili, ikiwemo kuimarisha mahusiano kwa lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi na kuchangia kukuza uchumi wa nchi yetu na hasa kupunguza umasikini kwa wafanyakazi watakaopata majanga yanayotokana na kazi zao," alisisitiza Dkt. Mduma.

Mafunzo hayo ya awamu ya nne yaliwaleta pamoja washiriki kutoka mikoa ya Ruvuma, Mtwara, Iringa, Mbeya, Songwe na Rukwa ambapo miongoni mwa mada zilizo wasilishwa ni kuhusu sheria ya fidia kwa wafanyakazi, taratibu za uwasilishaji na ushughulikiaji wa madai ya fidia kwa wafanyakazi.




Picha ya pamoja kati ya Jaji Kiongozi Mhe. Mustapher Siyani na baadhi ya Majaji Wafawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania waliohudhuria mafunzo hayo

# WCF yatoa msaada wa vifaa tiba

Na **Mwandishi wetu.**




Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma (kulia), akikabidhi sehemu ya msaada wa vifaa tiba kwa Mwenyekiti wa Chama Cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) Mkoa wa Dar es Salaam, Bw. Bernard Maro, kwenye ofisi ndogo za makao makuu ya WCF jijini Dar es Salaam.

Katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kuboresha huduma za afya nchini, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umekabidhi msaada wa vifaa tiba kwa Chama Cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) Mkoa wa Dar es Salaam.

Akipokea vifaa hivyo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, jijini Dar es Salaam Machi 4, 2024, Mwenyekiti wa TUGHE Mkoa wa Dar es Salaam, Bw. Bernard Maro aliishukuru WCF kwa msaada huo ambao ulikabidhiwa wakati wa wiki ya maadhimisho ya siku ya wanawake duniani.

Bw. Maro aliongeza kuwa wakati wote WCF imekuwa ni miongoni mwa taasisi za umma ambazo zimekuwa zikitenga sehemu ya bajeti zake kusaidia jamii kupitia sera ya kurudisha kwa jamii.

"Lakini pia katika utekelezaji wa Sheria yenu iliyouanzisha Mfuko, WCF imekuwa karibu sana na wananchi hasa wale wanaopaswa kupata huduma mnazotoa," alisema Bw. Maro na kuongeza kuwa kwa mujibu wa takwimu za TUGHE ambayo ina jukumu la kusimamia watumishi wa Serikali na Sekta ya Afya kutoka taasisi za Umma na Binafsi, WCF imekuwa ikitekeleza kwa vitendo masuala ya utawala bora, huduma bora na utekelezaji wa ushirikishwaji wa wateja wa Mfuko.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, alisema, Mfuko umekuwa na ushirikiano mzuri na chama cha TUGHE tawi la WCF, "Hili lazima niliseme mapema bila ya kusubiri 'forum' nyingine, TUGHE tawi wamekuwa na mchango mkubwa wa kutuletea mawazo ya kuboresha na kuimarisha taasisi yetu, wamekuwa ni watu wanaoongeza busara badala ya kuchochea moto pale panapokuwa na viashiria vinavyohitaji majadiliano," amefafanua.

Aidha Dkt. Mduma alibainisha kuwa ushirikiano kama huo umekuwepo kwani wanaamini kuwa chama hicho ni chombo muhimu cha kuusaidia Mfuko katika ngazi za mkoa na taifa ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wadau wa Mfuko kuelewa huduma zinazotolewa pamoja na haki zao.

"Kuhusu siku hii ya Wanawake Duniani, WCF imeamua kuwaunga mkono TUGHE ili kufikisha mahitaji muhimu kwa makundi mbalimbali yaliyoainishwa wakati huu wa maadhimisho ya siku Wanawake Duniani." Alisema Dkt. Mduma.

Siku ya Wanawake Duniani huadhimishwa tarehe 8 Machi ya kila mwaka.




Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma (kulia), akikabidhi sehemu ya msaada wa vifaa tiba kwa Mwenyekiti wa Chama Cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) Mkoa wa Dar es Salaam, Bw. Bernard Maro, kwenye ofisi ndogo za makao makuu ya WCF jijini Dar es Salaam.

# Bonanza la wafanyakazi WCF lafana, timu zagawana makombe



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Dkt. John Mduma akizungumza wakati wa ufunguzi wa Bonanza la Wafanyakazi Machi 24, 2024 katika viwanja vya michezo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.









■ Na **Mwandishi wetu.**

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umefanya bonanza la wafanyakazi ikiwa na lengo la kuimarisha afya pamoja na kuimarisha umoja na mshikamano miongoni mwa wafanyakazi.

Akifungua bonanza hilo lililofanyika tarehe 24 Machi 2024 jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa WCF Dkt. John Mduma aliwaeleza wafanyakazi hao kuwa michezo ni afya lakini pia ni nyenzo muhimu ya kuwaweka watumishi pamoja na kujenga umoja.

Dkt. Mduma aliwapongeza wafanyakazi wa WCF kwa kujitokeza kushiriki katika michezo mbalimbali kwa kuwa mbali na kufanya mazoezi ili kuimarisha afya zao na kupambana na magonjwa yasiyoambukiza pia michezo huchochea utimamu wa mwili na akili hivyo kuboresha utendaji wao.

Bonanza hilo lilishirikisha michezo mbalimbali ikiwemo mpira wa miguu, mpira wa pete, mpira wa kikapu, michezo ya jadi kama vile kuvuta Kamba, kukimbiza kuku, pamoja na chemsha bongo ya "team building".

Kwa mpira mguu kulikuwa na mtanange kati ya timu Dodoma Mkao Makuu, Dar es Salaam na Mikoani Combain ambapo timu ya Dar es Salaam iliibuka kidedeka kwa kupata pointi 4, wakifuatiwa na Dodoma ambao walipata pointi 3 na Mikoani pointi 1.

Kwa upande wa Mpira wa kikapu timu ya Dodoma iliicharaza timu ya Dar es Salaam kwa vikapu 10 dhidi ya 8, wakati kwa upande wa mpira wa pete timu ya Mkoa wa Dar es Salaam iliibuka mshindi mnono wa seti 22 dhidi ya 3 kwa timu ya Dodoma Makao Makuu

# Baadhi ya matukio wakati wa Bonanza la wafanyakazi wa WCF.














Mkurugenzi wa Huduma za Tathmini wa WCF Dkt. Abdulssaalaam Omar, akizungumza wakati wa mafunzo kuhusu vihatarishi vya udanganyifu (fraud) kwa wafanyakazi WCF yaliyofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 22 Machi 2024.



Baadhi ya watumishi wa WCF wakifuatilia mafunzo

# Watumishi WCF watakiwa kuwa waadilifu katika utendaji kazi wao

Na **Mwandishi wetu.**

Uongozi wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umewataka wafanyakazi wake kuzingatia misingi ya uadilifu wakati wote wa utumishi wao wa umma hususani wanapokuwa wanatekeleza majukumu ya kazi zao za kila siku.

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Huduma za Tathmini wa WCF Dkt. Abdulssaalaam Omar, alipokuwa akifungua mafunzo kuhusu vihatarishi vya udanganyifu (fraud) kwa wafanyakazi wote wa Mfuko huo yaliyofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 22 Machi 2024.

Dkt. Omar ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko huo Dkt. John Mduma katika ufunguzi huo, aliwaeleza wafanyakazi hao kuwa uadilifu wakati wanapotekeleza majukumu yao ndio msingi mkuu wa kuiwezesha WCF kufikia malengo yake ya utoaji wa fidia stahiki na kwa wakati kwa wafanyakazi wanaoumia au kuugua wakati wakitekeleza majukumu ya kazi zao.

"Kama watumishi ni lazima tuweke mkazo zaidi katika suala la uadilifu wakati wote tunapotekeleza majukumu yetu kwani ndio msingi mkuu wa mafanikio ya Taasisi yetu", alisema Dkt. Omar.

Aliongeza kuwa uadilifu ndio nguzo kuu inayobeba misingi mingine ya utendaji kazi ya Taasisi hiyo ikiwemo uweledi, uwajibikaji na ushirikiano. ***"Uadilifu ndio uti wa mgongo wa misingi yetu mingine, na kiukweli kama taasisi hatuwezi kufika popote kama hatutafanya kazi zetu kwa uadilifu mkubwa na kwa upande wa menejimenti tumejizatiti kuhakikisha tunaiishi misingi yote tuliyojiwekea na ndio maana mafunzo yakaandaliwa ili kukumbushana".***

Aidha, Dkt. Omar aliwasisitizia watumishi hao kujiepusha na vitendo vyovyote vya rushwa kwani havivumiliki kwa namna yeyote. "Kuhusu suala la rushwa kwa kweli halivumiliki (we have zero tolearance), na baada ya mafunzo haya hatutarajii kuona miongoni mwetu atokee mtu atakayebainika kujihusisha na vitendo vya rushwa au kuenenda kinyume na maadili ya utumishi wa umma", alisisitiza Dkt. Omar.

Katika mfunzo hayo ya siku moja yaliyohudhuriwa na watumishi wote wa WCF, mada mbili ziliwasilishwa kuhusu masuala ya maadili kwa watumishi wa umma pamoja na umuhimu wa watumishi hao kujiepusha na vitendo vya rushwa wanapokuwa wanatekeleza majukumu yao.



Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi Rasilimali Watu na Utawala WCF, Bw. Julius Lwenje akizungumza wakati wa mafunzo hayo.



# Wanawake WCF watoa msaada gereza la Segerea

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Bi. Laura Kunenge (Kulia) akikabidhi msaada wa mahitaji mbalimbali kwa Mkuu wa Sehemu ya Wanawake Gereza la Mahabusu Segerea SP. Hamida Matimba.

Na **Mwandishi wetu.**

Wafanyakazi wanawake wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) wametoa msaada wa mahitaji muhimu kwa wanawake mahabusu na wanaotumikia kifungo katika Gereza la Segerea Jijini Dar es Salaam ikiwa sehemu ya kurejesha kwa jamii katika kuelekea siku ya wanawake duniani, 2024.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano kwa Umma wa Mfuko huo Bi. Laura Kunenge alisema kwa kutambua majukumu makubwa anayobeba mwanamke kwenye jamii, wanawake wa WCF wameona ni vema kuwashika mkono wanawake wenzao ambao wana uhitaji.

"Tunafahamu kwamba serikali inafanya jitihada kubwa katika kuwahudumia wafungwa na mahabusu lakini na sisi tumeona katika kuadhimisha siku yetu tuwashike mkono wenzetu, WCF tunajua ukimsaidia mama umesaidia jamii nzima, na wenzetu waliopo hapa wakitoka watakuwa wamejifunza na watasaidia jamii zao, alisema Bi. Laura.

Kwa upande wake Mkuu wa Sehemu ya Wanawake Gereza la Mahabusu Segerea SP. Hamida Matimba alishukuru wanawake wa WCF kwa kuona umuhimu wa kuwakumbuka wanawake wenzao, na amesema kuwa msaada huo wa mahitaji muhimu utawasaidia sana wanawake hao hasa wale wenye watoto wadogo.

Siku ya Wanawake duniani huadhimishwa Machi 8 kila mwaka ambapo mwaka huu ilibeba kauli mbiu isemayo Wekeza kwa Mwanamke kwa Maendeleo ya Taifa na Ustawi wa Jamii.




Baadhi ya watumishi wanawake WCF walipofika Gereza la Segerea kukabidhi misaada

# Wafanyakazi wanawake WCF wapongezwa kwa utendaji kazi

Na **Mwandishi wetu.**

Wafanyakazi Wanawake wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) wamepongezwa kwa kuchangia kiasi kikubwa katika mafanikio ya Mfuko huo.

Pongezi hizo zimetolewa na Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi Rasilimali Watu na Utawala WCF, Bw. Julius Lwenje wakati wa hafla ya chakula cha usiku, iliyoandaliwa maalum kwa wafanyakazi wanawake wa Mfuko huo jijini Dar es Salaam.

"Nimepitia takwimu na kuona Idara ya Uendeshaji (Operations) asilimia 54 ya watumishi pale ni wanawake, na unapozungumzia uendeshaji mnajua ni pamoja na masuala ya uchangiaji na matekelezo, mafanikio ya Mfuko kwa kiasi kikubwa yamechangiwa na ninyi," alisema Bw. Lwenje na kuwataka kutokuridhika na sifa hizo na badala yake kuongeza bidii zaidi ya kazi kwa manufaa yao binafsi na Taasisi kwa ujumla.

Aidha, bwana Lwenje alisema asilimia 42 ya watumishi wote wa WCF ni wanawake, kiwango ambacho ni juu ya kile kilichowekwa chini ya muongozo wa kusimamia ulinganifu wa jinsia mahali pa kazi (Gender balance) ambao unataka walau asilimia 30 ya watumishi wawe ni wanawake.

Kwa upande wake, Mshauri wa masuala ya kisaikolojia, Bi. Sadaka Said, alisema jamii inaamini siku zote wanawake ni wapambanaji lakini katika mchakato huo wa upambanaji wanajikuta wanajisahau na kuangalia wengine.

Alifafanua kuwa kutokana na hali hiyo mwisho wa siku wanawake wanajikuta wamechoka na kushindwa kuendelea na harakati za kujikwamua kiuchumi. "Huanguki physically ila unajikuta moyo umeelemewa na hapa ndio unakuja umuhimu wa kujipa thamani yaani self-love." Alifafanua Bi. Sadaka.

Aidha aliwataka wanawake kujipa thamani na kufanya mambo kulingana na vile wanavyotaka. "Tunapozungumzia kufanya kile unachotaka, tunamaanisha kuwa kila unachokifanya hakikisha hakimkwazi mtu, huingii kwenye nyumba ya mtu, huingii kwenye paa la mtu, bali unasimama kama wewe, unajidhibiti mwenyewe na unajua unachokitaka," alisisitiza.

## Matukio mbalimbali wakati wa hafla ya chakula cha jioni kwa wafanyakazi wanawake WCF











WCF
Workers Compensation Fund

# WCF ONLINE SELF SERVICE PORTAL

https://portal.wcf.go.tz

## Pata Huduma za WCF Mtandaoni

1. Online employers' registration & issuance of eletronic certificate (Usajili wa waajiri na hati ya usajili)
2. Online payment of contribution through generation of control numbers & issuance of electronic receipts (Kuwasilisha michango ya kila mwezi kupitia namba ya udhibiti na kupata stakabadhi)
3. online changes of employees' and employers' particulars (Kuhuisha taarifa za wafanyakazi na mwajiri)
4. Online submission of return of annual earnings (Kuwasilisha Taarifa ya Mapatoya Mwaka ya Wafanyakazi)
5. Online submission of notification for occupational accidents, diseases and deaths (Kuwasilisha taarifa ya ajali, ugonjwa ama kifo kitokanacho na kazi)
6. Online claims tracking (Kupata mrejesho wa madai ya fidia)

*"Adequate and Equitable Compensation"*

www.wcf.go.tz | info@wcf.go.tz | 0800 11 00 28

**Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)**

Jengo la Kambarage,
Ghorofa ya 3,
S. L. P 329, 41104 Dodoma.

info@wcf.go.tz www.wcf.go.tz 0800 11 00 28